

Pambazuko

Toleo Namba 0046

Jumatatu Septemba 11-16, 2023



Tope la kashfa NHIF

Uk. 9

Waziri wa Afya Ummu Mwalimu

● *Yadaiwa kuingilia faragha za wagonjwa*

Lissu: Hatukomi, hatuogopi

Uk. 10



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Siyo vigogo tu, wastaafu watunzwe

SERIKALI ya Tanzania iko mbioni kuanza kulipa mafao kwa wenza wa viongozi wakuu wastaafu ama wale waliofariki dunia.

Viongozi wakuu wanaotarajiwa kuguswa na sheria hiyo itakapopitishwa na Bunge, hatimaye kuanza kutumika baada ya rais kuridhia, ni pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, makamu pamoja na waziri mkuu.

Wiki iliyopita, mchakato wa kuwepo kwa sheria hiyo ulianza, ambapo muswada wake ulisomwa kwa mara ya kwanza bungeni, jijini Dodoma.

Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson alilileza Bunge kwamba muswada huo baada ya kusomwa kwa mara ya kwanza, utapelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa ajili ya kuchambuliwa kabla ya kurejeshwa bungeni kuendelea na hatua zingine, ikiwamo kusoma kwa mara ya pili.

Sambamba na hatua hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aliliambia Bunge kwamba serikali inatarajia kufanyia marekebisha baadhi ya stahiki na mafao ya majaji – kwa maana ya kuyaboresha.

Pambazuko linapenda kuweka msimamo wake sawia; kwamba limefarajika kuona kwamba serikali imenuia kuhakikisha viongozi wastaafu (walio hai au waliofariki dunia) ama wenza wao wanaendelea kufurahia utumishi wao kwa umma wa Tanzania, wakiwa nje ya ofisi – kutokana na umri, ugonjwa ama sababu zingine zinazotajwa na Katiba, kuondoka madarakani.

Pamoja na nia hiyo njema ya serikali, lakini Pambazuko halijasoma mahali popote nia ya serikali kuongeza stahiki yoyote kwa watumishi wengine wa umma ambao wametumia zaidi ya asilimia 75 ya umri wao kulitumikia taifa.

Sisi tungependa kushauri kwamba - serikali inapofikiria kuongeza stahiki kwa watumishi “vigogo” ama mafao kwao na wenza wao, basi ingefikiria pia namna ya kuongeza mafao na hata stahiki kwa watumishi na wastaafu wote mtawalia; wa serikali bila kujali dhamana zao.

Kuwajali watumishi wote wa umma – kwa kuwaongeza stahiki na mafao, kutaonyesha namna serikali isivyokuwa na ubaguzi wa dhamana, hivyo kujenga taswira ya kuwajali wanapokuwa kazini na hata baada ya kustaafu.

Pambazuko linapendekeza kwamba kuanza kwa mchakato wa kuongeza mafao kwa viongozi wastaafu na wenza wao, kuende sambamba na taarifa za kuanza kwa mpango wa kuongeza mafao na stahiki kwa wengine pia.

Hili likifanyika, umma utaelewa kwamba Tanzania ni nchi yenye usawa na kwamba haipendelei wenye dhamana tu, ambao uhakika ni kwamba wana ukwasi wa kutosha; wakiwa madarakani na hata baada ya kustaafu.

Ni dhahiri viongozi wetu; rais, makamu wake na waziri mkuu, wanapokuwa madarakani wanapata stahiki kufuru nyingi mno zinazowapa ‘jeuri ya maisha’ hata baada ya kustaafu.

Wakati ni sasa wa kuweka mazingira ya usawa; ya mafao na stahiki zingine, kwa watumishi wote.

CHEKO LA SAMIA...



Rais Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo na Naibu Kiongozi wa Masuala ya Maendeleo ya Kiuchumi Afrika kutoka Idara ya Pan-Africa, Uingereza, Mansoor Ahmad wakati wa hafla ya chakula cha jioni alichowaandalia viongozi kutoka mataifa mbalimbali waliohudhuria mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) Ikulu Jijini Dar es Salaam. Hafla hiyo ilifanyika Septemba 7, 2023. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Mtu mwenye mafanikio ni yule anayeweza kujenga msingi imara wa maendeleo kwa kutumia matofali yaliyotupwa na wengine -David Brinkley (mtangazaji maarufu wa vipindi vya redio Marekani).

Ikulu inakwama wapi?

Na Igo AI

HADI leo alfajiri – Jumatatu, Septemba 11, saa 6:17 usiku, Tovuti Rasmi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilikuwa na makosa mengi ya kiutendaji na usimamizi.

Tovuti hiyo yenye anwani hii: www.ikulu.go.tz; ilikuwa ikionesha kwamba mawaziri waliobadilishwa ama kuondolewa kwenye baraza la mawaziri, bado wanahudumu kwenye nafasi zao.

Hatua hii ya kutobadilisha vyeo vya

mawaziri ama kuwepo kwa walioachwa katika uteuzi siku 10 zilizopita, ni makosa ambayo yanapaswa kurekebishwa haraka.

Katika tovuti hiyo, Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Biteko, anatajwa kuwa ni waziri wa madini, cheo ambacho mabadiliko ya Agosti yamemuamisha. Hivi sasa pamoja na kuwa naibu waziri mkuu, pia amwekuwa waziri wa nishati.

Waziri wa Madini kufuatia mabadiliko hayo ya baraza, ni Anthony Mavunde, ambaye awali alikuwa Naibu Waziri wa Kilimo.

Inaendelea Uk. 5



MHE. SAMIA SULUHU HASSAN
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



MHE. DKT. PHILIP ISDORA MPANGO
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



MHE. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi



MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Uvuwaj



MHE. DKT. DOTO MASHAKA BITEKO
Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini



MHE. KAPT. GEORGE HURUMA MKUCHIKA
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu (Kazi Maalum)



MHE. GEORGE B. M. SIMBACHAWENE
Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora



MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uvuwaj



MHE. INNOCENT L. BASHUGUWA
Waziri wa Ulinzi



MHE. ANGELLA J. KAIRUKI
Waziri wa Maliasili na Utalii



MHE. SELEMAN S. JAFU
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)



MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)



MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA
Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi

Ikulu inakwama wapi?

Inatoka Uk. 4

Tovuti hiyohiyo inamtaja Dkt. Angeline Mabula kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakati aliondolewa katika nafasi hiyo na sasa anaendelea kuwa mbunge. Nafasi ya Mabula ameteuliwa Jerry Silaa.

Innocent Bashungwa, ambaye sasa ni Waziri wa Ujenzi, tovuti hiyo, bado inamtaja kwamba ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kitu ambacho siyo kweli.

Zaidi sana, tovuti hiyo ya ofisi nambari wahedi, inamtaja Prof. Makame Mbarawa kuwa bado ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, wakati ukweli ni kwamba profesa huyo sasa ni Waziri wa Uchukuzi.

Jicho la Tai, safu mpya ya Pambazuko ambayo inajikita kurekebisha mahali ambapo kuna kulegalega kwa mambo.

Lengo kubwa siyo kukomoa ama kuonea, bali kutonya mahali ili hatua za haraka zichukuliwe kabla ya mambo hayajaharibika.

Kama jina la safu hii linavyojieleza, Jicho la Tai; ni kiungo muhimu kwa ndege tai katika kusaka chakula na kupenya na kubaini maadui kwa kujilinda hata kutokea mbali.

Safu hii, inabeba jicho hilo katika kuona na kung'amua wapi kuna pwaya, kuna mkwamo na kuwatonya wahusika na hasa wafanya uamuzi kuchukua hatua za haraka kuokoa jambo.

Mfano mzuri ni hii Tovuti Rasmi ya



MHE. UMAYY A. MWALIBU
Waziri wa Aya



MHE. JENETTA J. MHAGAMA
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)



MHE. DKT. MWIGULU N. MADELI
Waziri wa Fedha



MHE. MHANDEI HAMAD Y. MASABUNI
Waziri wa Mambo ya Ndani



MHE. DKT. STEROMENA LAWRENCE TAY
Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa



MHE. HUSSEIN BASHE
Waziri wa Kilimo



MHE. ABDALLAH H. ULEGA
Waziri wa Mifugo na Uvuvi



MHE. PROF. ADOLF F. MKENDA
Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia



MHE. NAPE M. NHAUYE
Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari



MHE. JANJARI Y. MAKAMBA
Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Barabara



MHE. DKT. ANGELINE SYLVESTER LUPALA MABULA
Waziri ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi



MHE. DKT. DAMAS D. NDIKUMBAHO
Waziri wa Uhamaduri, Sena na Michezo



MHE. DKT. DOROTHY O. GIBRAMA
Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wamwazi na Mafundisho



MHE. DKT. ASHATU K. KULJI
Waziri wa Viwanda na Biashara



MHE. JUMA H. AMESO
Waziri wa Maji



MHE. DKT. PIPHI H. CHAMA
Waziri wa Sheria na Katiba



MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMBAZUKU)

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo hadi leo; ikiwa ni siku 10 tangu Agosti 30 – baraza lilipobadilishwa, bado inabeba wasiokuwamo au kubadilishwa.

Hii maana yake ni kwamba kuna kupwaya katika uendeshaji wa tovuti hiyo, hivyo kuwa na taarifa ambazo siyo sahihi kwa wanaoitembelea.

Ni vyema basi, wahusika wabadilishe haraka vyeo halali vya mawaziri ili kuweka taarifa na kumbukumbu sahihi za dhamana za viongozi waliopo.

Siku njema kwa wote.

Habari

Usiri wa nini Bandari ya Zanzibar?

NaJabir IDRISSE,
Zanzibar

KUMEKUWEPO usiri mkubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kueleza umma kuwepo kwa mchakato wa kumpata mwekezaji katika bandari kuu ya visiwa hivyo.

Hata hivyo, mwishoni mwa wiki iliyopita, kumepatikana tangazo kupitia mitandao ya kijamii likieleza kwamba shughuli zote za uendeshaji wa Bandari ya Zanzibar zitakuwa chini ya mwekezaji.

Tangazo hilo linaeleza kuwa Jumatatu ijayo, Septemba 18, 2023, shughuli zote za uendeshaji Bandari ya Zanzibar, zinakabidhiwa kwa mwekezaji.

Tangazo hili ni dhahiri limetokana na maridhiano na matakwa ya taasisi mbili; Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC), menejimenti ya bandari kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na mwekezaji.

Hili tangazo lipo katika vyombo ya habari vya kidigitali - Twitter, Instagram na Facebook, lina viwakilishi vya taasisi hizo, wawakilishi wa Serikali, na Africa Global Logistics (AGL), kampuni inayobeba hisa ya wawekezaji.

Hakuna taarifa zaidi wala ufafanuzi wa kuujulisha umma asili na mantiki ya suala lenyewe la ushirikiano huu mpya.

Hata hivyo, ni dhahiri kwamba kinachofuata baada ya tangazo, ndio kuanza kwa utekelezaji wa makubaliano, wengine wakiita ni mkataba wa uendeshaji bandari, kwa mfumo mpya wa kushirikisha sekta binafsi.

Kumekuwepo na fununu hizi kwa muda, kiasi kwamba wananchi wa Zanzibar wamesikika wakilalamika kwa kutopewa taarifa tangu awali.

Imefahamika kuwa AGL ni kampuni ya wageni. Hawa ni wawekezaji kutoka Ufaransa, awali hawakusajiliwa Zanzibar wala kwa sheria ya kampuni ya Jamhuri



Rais Hussein Mwinyi

ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, baada ya malalamiko ya wananchi kusikika, baadhi ya viongozi wa Zanzibar, walianza kuibuka kwa kueleza kuwepo kwa “ufanisi mkubwa” katika bandari endapo mwekezaji atapatikana.

“Utatokea wapi utendaji babaishi wakati sasa tutakuwa na wawekezaji wageni kuiendesha bandari yetu, na hii itakuwa ni muarubaini wa matatizo makubwa na madogo,” amesikika akisema kiongozi mmoja alipoulizwa kuhusu maoni yake juu ya uwekezaji huu.

Huku akikataa kutajwa jina gazetini, amesema itakuwa bahati mbaya ikiwa wawekezaji hao wageni watashindwa kubadilisha mambo na hivyo kukosa kuchagiza ufanisi kwenye utendaji.

Tangazo hilo linaonekana ikiwa ni miezi mitatu kupita baada ya kuwepo hafla katika Ikulu ya Zanzibar ambapo alionekana Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi akishuhudia utiwaji saini wa mikataba kadhaa ambayo hata hivyo haikuelezwa ilihusika na nini.

Katika televisheni ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), alionekana Rais Mwinyi akiwa na wasaidizi wake pamoja na baadhi ya viongozi wa usimamzi wa bandari.

‘Kwita Izina’ kupaisha utalii

Na Nestory NESTORY

RWANDA imeendelea kujipambanua kuwa na dhamira ya dhathi ya kuendelea kukuza mawanda machache ya utalii wake kwa kutumia watu maarufu duniani, wengi wakitokea Marekani, Ulaya na Asia.

Mkakati wa nchi hiyo umefanikiwa kuwapata wacheza sinema, masumbwi, mieleka na hata kandanda.

Hivi karibuni, Rwanda iliwapata waigizaji maarufu wa Marekani, Idris Elba na Kevin Hart na kuwateua kuwa mabalozi ambao watakuwa na kazi moja kubwa; kuwapa sokwe majina ili waendeleo kuwa kivutio cha watalii.

Wakiwa nchini Rwanda hivi karibuni, watu hao maarufu waliungana na serikali ya nchi hiyo katika sherehe ya kuwapa majina wanyama hao. Sherehe hiyo inayoitwa “Kwita Izina” – maneno ya Kabila la Watusi yaani kuwapa majina – kwa Kiswahili.

Elba na Hart waliungana na viongozi wa serikali na wageni kutoka nchi mbalimbali katika eneo maarufu la Hifadhi ya Kitaifa ya Volcano huko Kinigi, Musanze, kwa ajili ya sherehe maalumu ya kuwapa sokwe majina.

Katika kipindi cha miezi tisa, jumla ya sokwe 23 waliozaliwa na hawa ndiyo waliopewa majina.

“Kwita Izina siyo tukio tu, ni heshima kwa sokwe wa milimani na jumuia zilizojitolea kutetea uhifadhi wao,” Clare Akamanzi, alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Maendeleo ya Rwanda.

Rwanda ilianza kuwapa majina sokwe wa milimani mwaka 2005, katika kile ambacho kimekuwa sasa sherehe ya asili ambayo hufanyika kila mwaka.

Jumla ya sokwe watoto 374 wamepewa majina tangu Kwita Izina ya kwanza kufanyika.

Clare anaeleza kuwa kuwapa majina



Sokwe

sokwe, kumeendelea kuwa maarufu na sasa Rwanda inapokea watalii wengi zaidi kila mwaka. Kwamba wapo wanaokuja kushuhudia shughuli za kuwapa majina wanyama hao zinavyofanyika na wengine wakipendezwa na mazingira, maisha ya Wanyarwanda na vivutio vingine.

Utaratibu huu wa kuwapa majina wanyama wakubwa umeanza kuwa maarufu maeneo mengi duniani, na baadhi ya nchi za Afrika “zimeubeba kwa kasi.”

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, mbali na kubariki utaratibu huu, alibuni njia nyingine ya kuitumia timu ya kandanda ya Arsenal, ya England kutangaza na kuhimiza dunia kutembelea Rwanda. Jezi za timu hiyo zinabena maneno haya; Visit Rwanda (tembelea Rwanda kwa Kiswahili).

Miongoni mwa nchi ambazo zimeanza kuweka msisitizo kwa kuwapa majina ya watu wanyama wakubwa ni Tanzania na Afrika Kusini. Baadhi ya wanyama wanaopewa majina katika nchi hizo ni simba, tembo, faru na twiga.

Utaratibu unaotumika kuwapa majina wanyama hao ni pamoja na kuchangia fedha kwa ajili ya jina na zaidi sana katika Tanzania, mwenye jina lake kwa mnyama anapaswa kuchangia fedha kiasi kila mwaka kwa ajili ya kumlinda.

Tangazo

Ukiwa Bukoba...

Furahia Nene Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya;

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Waziliana nazi kwa
namba hii:

0753949488



Tope la kashfa NHIF

Na Mwandishi WETU

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya Tanzania (NHIF) umeingia katika tope zito la tuhuma kwamba unaingilia faragha za wagonjwa wanaotibiwa kwa kadi zake.

Tuhuma hizo ambazo hata hivyo NHIF imekataa kujihusisha nazo, zinahusu wagonjwa kupigiwa simu na kuhojiwa maswali kadhaa ambayo kimsingi yanaingilia faragha ya mgonjwa kinyume cha sheria na taratibu za afya.

Pambazuko, gazeti ambalo limefuatilia tuhuma hizi baada ya kupokea taarifa za kuwepo kwa “utaratibu huo mpya” wa kuhakiki madai ya hospitali binafsi kwa NHIF baada ya kutoa huduma kwa wagonjwa.

Baada ya kuhojiwa na Pambazuko kuhusu madai hayo makubwa, kiongozi mmoja mwandamizi wa mfuko huo alishindwa kukataa ama kukubali, na kuhoji; “nyie mmepata wapi taarifa hizi?”

Kiongozi huyo aliyekataa kutajwa jina lake gazetini, alisema mfuko wao hauwezi kuruhusu taarifa za wagonjwa kujadiliwa kwa watu wasiokuwa madaktari ama wataalamu wa afya wengine ambao wameidhinishwa na sheria.

“Mimi kamwe siwezi kueleza lolote kuhusu wagonjwa, nyie kama mmepata taarifa zenu kutoka mnakojua, endeleeni, lakini sisi hatuna utaratibu huo,” aliongeza kwa sauti iliyosikika kubeba lafudhi yenye ukali.

Pambazuko lilielezwa na baadhi ya wamiliki wa hospitali binafsi – walioko Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, kuwepo kwa ukweli wa tuhuma hizo na kwamba hali hiyo imegeuka kuwa usumbufu mkubwa kwa wagonjwa wao.

“Ndiyo tumeulizwa sana na baadhi ya wagonjwa kuwepo kwa watu wanaowapigia simu kutaka kujua endapo

walipewa huduma katika hospitali zao,” alieleza daktari mmoja kutoka eneo la Mabibo, Dar es Salaam.

Huku akikataa kutajwa jina lake gazetini kwa kuwa bado hajalipwa, hivyo kuhofia kukwama kwa malipo yake kutoka NHIF, daktari huyo alisema baadhi ya wagonjwa wake wameeleza kuhojiwa maswali ambayo mengine yanaingilia faragha ya wagonjwa.

Pambazuko limeelezwa baadhi ya maswali yanayoulizwa na hao wanaodai kuwa maofisa kutoka NHIF ni; jina la mgonjwa; je, alitibiwa wapi na lini; je, aliandikiwa gharama za matibabu yake; je, alipewa dawa gani ama kupata huduma nyingine; je, alikuwa anaumwa nini na zaidi mahali anakofanya kazi yeye ama ndugu yake ambaye ndiye mmiliki wa kadi ya bima.

Juma Kihale, mwanasheria ambaye alizungumza na Pambazuko alisema ni kosa kubwa wa NHIF kuhoji mashwa hayo kwa wagonjwa, kwani yanaingilia moja kwa moja faragha ya mgonjwa.

“Endapo kuna ukweli wa mambo haya, ni hatua mbaya sana kuwahi kutokea katika historia ya mfuko huo wa afya,” ameongeza mwanasheria huyo anayeendesha shughuli zake Dar es Salaam na kuongeza; “hata kama wanataka kuhakiki madai, hawana haki ya kuingilia faragha za wagonjwa.”

Mwanasheria huyo anasema kuwa uwezekano mkubwa kwamba wanaopiga simu ni maofisa wa NHIF wenyewe au watu wenye ukaribu nao, wanaochukua taarifa za wagonjwa na kuwasumbua, kwa malengo wanayojua wao.

Hata hivyo, imebainika kuwa wanaopiga simu kwa wagonjwa wanaotumia kadi za bima za mfuko huo, hawaombi pesa wala kuhitaji kitu chochote, isipokuwa taarifa za mgonjwa

Habari**Lissu: Hatukomi, hatuogopi**

Na Nestory NESTORY

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) huenda akaendelea kuweka historia ya kuwa mwanasiasa anayekamatwa mara kwa mara na Jeshi la Polisi.

Mbali na historia hiyo, huenda pia akavunja rekodi ya kuachiwa mara kwa mara kwa dhamana ya Polisi, kabla ya kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma.

Katika kamatakamata hizo na kuachiwa, tuhuma kubwa ni uchochezi, kukaidi amri halali na pia kuzuia Polisi kutekeleza majukumu yake.

Tangu Julai, 2016 hadi Septemba 10, mwaka huu, amekamatwa, kuhojiwa na kuachiwa na Polisi mara 11.

Mapema jana, Jumapili ya Novemba 10, Lissu alikamatwa na Jeshi la Polisi Mkoani Arusha na kuhojiwa kabla ya kuachiwa saa 2:30 usiku.

Lissu pamoja na viongozi wenzake wa Chadema walikamatwa Mjini Karatu katika Hoteli za Ngorongoro Crater na Panorama jana na kushikiliwa na jeshi hilo kwa mahojiano.

Kabla ya kukamatwa, askari Polisi ambao idadi yao haikujulikana mapema kwa Pambazuko, jana asubuhi walizingira hoteli hizo kwa lengo la kuwatia nguvuni viongozi hao wa Chadema waliotarajiwa kufanya mkutano wao wa hadhara katika Mji wa Karatu.

Baada ya kuachiwa jana usiku, Lissu alitisha mkutano na wandishi wa habari kueleza kilichotokea na hatua zinazofuata baada ya kupewa dhamana na jeshi hilo lenye majukumu ya kulinda raia na mali zao.

Katika kikao hicho, Lissu alisema kwamba Jeshi la Polisi lilimhoji kuhusu tuhuma za kuendesha mkutano bila kibali na kwamba alikuwa akituhumiwa pia kuzuia askari Polisi kutekeleza



Tundu Lissu (mwenye miwani, aliyekaa) katikati, akizungumza na waandishi wa habari jana usiku baada ya kuachiwa kwa dhamana na Jeshi la Polisi, Arusha. (Picha kutoka Chadema).

majukumu yao.

Pamoja na madhila hayo ya kukamatwa, Lissu na wenzake wameapa kwamba wataendelea na ratiba ya mikutano yao ya hadhara katika Mkoa wa Arusha.

“Hakuna mahali Katiba ya Tanzania inazuia wananchi kukutana ama vyama vya siasa kufanya mikutano yake, sasa iweje sisi tuzuiwe kuzungumza na wanachama na mashabiki wetu, hii haikubaliki,” alisema Lissu.

Lissu alisema kwamba wao hawatakoma wala kuogopa kukamatwa kwani “mapambano ya kueleza ubaya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)” hayana ukomo, na kuwa Chadema kitaendelea kufanya kazi hiyo kwani hakivunji sheria yoyote ya nchi.

Lissu ambaye pia ni mwanasheria mkuu wa Chadema, alikamatwa pamoja na viongozi wengine waandamizi wa chama hicho cha upinzani alisema sababu kubwa ya kukamatwa kwao ni kuwazuia kufanya mikutano yao ya hadhara.

“Hawa walitukamatwa kwa lengo moja tu; kuzuia tusifanye mikutano yetu Ngorongoro na maeneo mengine ambako kuna ukikukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaoendelea kufanywa na watawala,” aliongeza.

Bukoba Raha

... Bukoba kuna senene
... Bukoba kuna maji safi na salama

**Lakini Bukoba kuna G-smart Sauna & Steam Bath
(Bafu la kuoga kwa mvuke).**

**Ukiwa Bukoba ama unaishi, usisahau
kupata huduma G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Hakika hautajuta na ona fahari kusimulia
wengine huduma za G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Faida za Sauna na Steam Bath ni nyingi,
lakini chache ni zifuatazo:**

- Inaboresha afya ya moyo na mishipa
- Huondoa uchovu wa mwili na misuli
- Kuondoa msongo wa mawazo (stress)
- Kuzuia magojwa ya kukakamaa kwa misuli
- Inaboresha na kuhuisha mfumo wa usingizi
- Kuondoa sumu na kufanya ngozi nyororo zaidi

**Wasiliana na G-smart and Steam Bath
walioko Barabara ya Kashozi na wapigie
simu kwa namba: 0626 265725 / 0767 291 670**

Habari**Ujerumani kubana matumizi zaidi****Na Mwandishi MAALUM**

DUNIA hivi sasa inakabiliwa na hali ngumu ya uchumi. Siyo Afrika wala Bara Hindi pekee, hata nchi tajiri zimeanza kuona “cha moto.”

Njia rahisi ya kudhibiti hali ngumu ya uendeshaji wa serikali na kujali huduma za jamii kwa nchi, ni kubana matumizi kadri inavyowezekana.

Matumizi makubwa, hasa yasiyogusa maendeleo ya moja kwa moja ya nchi husika, yameanza kudhibitiwa na nchi tajiri.

Sasa ni zamu ya Ujerumani ambayo taarifa zinaeleza kwamba imeanza mchakato wa kubana matumizi makubwa katika bajeti yake.

Ikumbukwe kwamba miaka mitatu iliyopita, Ujerumani – kama ilivyokuwa kwa dunia nzima, ilikabiliwa na athari za janga la Covid-19 na baadaye mzozo wa kivitani kwenye Ukraine, hivyo kuingia katika matumizi makubwa ya fedha kujihami.

Katika kufanya hivyo, nchi hiyo ikaingia kwenye wigo wa madeni makubwa na sasa inahaha kupunguza deni lake la taifa.

Waziri wa fedha wa nchi hiyo, Christian Lindner kutoka chama cha kiliberali, FDP, anatumai kukomesha miaka kadhaa ya matumizi makubwa na kupanda kwa gharama ya nishati.

Rasimu ya bajeti ya nchi hiyo inatarajiwa kufikia euro bilioni 445, sawa na dola bilioni 480 kwa ajili ya mwaka ujao wa 2024, ikiwa pungufu la euro

bilioni 30 kutoka bajeti ya mwaka huu wa 2023, lakini iko juu kwa takribani euro bilioni 90 kuliko ya mwaka 2019.

Bajeti ya mwaka 2019 ndiyo ilikuwa bajeti ya mwisho kabla ya kuzuka kwa janga la Covid-19. Pamoja na hayo, karibu idara zote za serikali zitalazimika kubana matumizi ikilinganishwa na mwaka uliyopita.

Waziri Lindner anabainisha kuwa bajeti ya 2024 inahusisha kiasi cha euro bilioni 16.6 katika mikopo mipya, ikiwa ni euro bilioni 30 chini kuliko mwaka huu.

Akitetea mipango yake wakati wa majadala wa wazi wiki iliyopita, Lindner alitaja matumizi yanayoongezeka kwa kasi ya kulipia deni.

Waziri huyo alisema malipo ya riba pekee yataigharimu serikali yake euro bilioni 37.

Kwamba gharama za riba katika bajeti hivi sasa zimefikia mara mbili zaidi ya bajeti ya waziri wa elimu na utafiti, na kuongeza kuwa “hatuwezi kumudu madeni yasiyokuwa na udhibiti ambayo ni vigumu kuyagharimia.

Makato hayo ni tata kwenye serikali ya shirikisho ambayo muungano wake unahusisha chama cha Kansela Olaf Scholz, ambacho kinafuata siasa za mreno wa wastani wa kushoto, cha Social Democratic (SPD).

Chama kingine ambacho kinaungana na SPD ni chama cha watetezi wa mazingira cha Die Grüne, ambavyo vyote vinaunga mkono suluhisho la kuingilia kati kwa utatuzi wa matatizo ya kiuchumi nchini Ujerumani.

100% TRUSTED BRAND



DOR EASY WASH

LIQUID SOAPS

**USAFI WAKO
NI JUKUMU LETU**

MANUFACTURED BY: DOR EASY WASH
P.O BOX 80159 KIBADA, KIGAMBONI | DAR ES SALAAM - TANZANIA
MOB: +255 715 771 123 | EMAIL: DOREASYWASH@GMAIL.COM

Habari

Tope la kashfa NHIF

Inatoka Uk. 9

husika.

Ifahamike kuwa hospitali zinapopeleka madai NHIF ya kulipwa fedha zao baada ya kutibu wagonjwa, hutumia fomu ambazo zina taarifa zote za mgonjwa aliyehojiwa na hospitali husika.

Pambazuko limeona fomu hizo na kuhakiki kwamba zinabeba taarifa za mgonjwa, mahali alipotibiwa, dawa alizopewa na gharama zake.

NHIF hadi sasa inalalamikiwa kwa kusuasua kulipa madai ya hospitali zinazohudumia wagonjwa wa kadi zake za bima, inaelezwa kuelemea kwa madeni makubwa, hivyo kuhofia “uhai wake.”

Hata hivyo, mara kwa mara inapotajwa kwamba mfuko huo upo hoi kifedha, viongozi wake, na hata serikali, imekuwa ikijitetea ama kutetewa kwamba “iko imara kiuchumi.”

Mbali na kulalamikiwa na wagonjwa, NHIF imeelezwa kukata kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwenye madai ya wamiliki wa hospitali binafsi wanaohudumia wanachama wa mfuko huo.

Kutokana na hali hiyo, yapo madai kwamba hospitali nyingi binafsi zimefunga kutoa huduma au kukataa kupokea wagonjwa kwa mfumo huo wa bima ya taifa.

Inadaiwa kuwa mfumo huo wa bima ya afya ulioanzishwa kisheria, umekuwa ukikata kati ya asilimia 25 hadi 50 kwa kila madai yanayotoka kwa watoa huduma.

Mmiliki wa zahanati moja jijini Mwanza ambaye hakupenda kutaja jina lake amesema baadhi ya watendaji wa NHIF wamekuwa na utaratibu huo ambao ‘unawaumiza’ wamiliki wa zahanati na hospitali binafsi.

Mmiliki huyo alidai kuwa akipeleka madai Sh. milioni 17, NHIF hukata kiasi cha Sh. milioni tatu au zaidi,



Kadi za Bima za NHIF

jambo ambalo linawatia hasara kubwa kuhudumia wananchi wagonjwa.

Kiongozi mmoja wa NHIF alipohojiwa na mwandishi wa habari hizi, alikanusha na kueleza kwamba madai yao hayana msingi kwani shughuli zote za uhakiki wa malipo hufanywa kwa uwazi na penye matatizo wamiliki uhusishwa.

Uchunguzi umebaini kwamba kutokana na sababu hizo, baadhi ya wamiliki wa hospitali wamekuwa wakikataa kuwatibu wagonjwa wenye kadi za NHIF na wengine kukataa kutoa baadhi ya huduma, ikiwamo zile zenye gharama kubwa.

Inaelezwa sababu kubwa kwa baadhi ya hospitali kushindwa kutoa huduma au dawa zenye gharama kubwa ni NHIF kugoma kulipa huduma hizo wanapopelekewa madai.

Kwamba madai hayo halali, hutolewa katika orodha ya malipo kwa maelezo kwamba “hakukuwa na sababu kwa hospitali kuwapa wagonjwa dawa au huduma hizo.”

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Benard Konga, alipoulizwa kuhusu kuwepo kwa adai hayo, alikiri kukumbana nayo, lakini akaeleza wengi wanaolalamika hukosea kufuata masharti na taratibu za makubaliano ya mkataba baina ya mfuko na wamiliki binafsi wa hospitali.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Makala

Rais Samia ni fursa, asitwezwwe

Na Rashid MTAGALUKA

TANGU Machi 19/2021 Rais Samia Suluhu Hassan alipoapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mpaka sasa, amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga heshima binafsi na nchi yetu.

Rais Samia alikula kiapo hicho kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Dkt. John Pombe Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, 2021 katika hospitali ya Mzena jijini Dar Es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu.

Katika hotuba zake, Rais Samia mara kadhaa amekuwa akisisitiza kuwa, yeye na Magufuli hawakuwahi kutofautiana mahala, ndiyo maana katika salamu yake alisema kiitikio kiwe “Kazi iendeleo”

Hivyo, katika hali ya kawaida hatutarajii mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu kwa njia yoyote ile iwayo, waamuwe iwe kwa makusudi au bahati mbaya, kufanya jambo litakaloashiria moja kwa moja, ama kwa taathira yake - kushusha heshima ya Rais Samia.

Ndiyo maana wapo wengine wakibaini kuna mambo serikalini ama ndani ya chama chake – Chama Cha Mapinduzi (CCM), yanakwenda katika namna ya “kufunika kombe mwanaharamu apite,” wanaamua “kufunua kombe ili mwanahalali asimame” hata kama tunajua kufanya hivyo kutatugharimu.

Hii ni baada ya kutambua kwamba, maisha yetu hayana thamani sana kuliko iliyo thamani ya heshima, utu na uzalendo wa rais wetu ambaye ni nembo ya taifa letu la Tanzania.

Ukisoma Katiba ya CCM ukurasa w mwisho utaona mahala pameandikwa kwa herufi kubwa ‘NYONGEZA A’

Chini ya maneno haya utakutana na ahadi tisa za mwanachama wa CCM ambazo zimerithiwa kutoka Tanganyika African National Union (TANU).

Ahadi nambari nane inasema hivi;



Rais Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa CCM

“Nitasema kweli daima fitina kwangu mwiko,” mwisho wa kunukuu.

Ingawa sina kumbukumbu iwapo ahadi hii imewahi kufutwa na kikao chochote halali cha CCM au la, lakini wana CCM wenyewe hawataki kuifanyia kazi wakihofia kuvishwa joho la usaliti wa chama, mpinzani au mamluki unayetumika kukivuruga chama chao.

Kukosekana kuifanyia kazi ahadi hii muhimu kwenye CCM, ndiyo maana leo tunashuhudia kuibuka kwa makundi ya watu wanaojipendekeza kwa viongozi wa juu kila kona wakilenga mlo wa siku pamoja na nafasi za uteuzi,

Inasikitisha kuona wimbi hilo limewakumba mpaka vijana wasomi kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini ambao tungetaraji kiwango cha elimu walichonacho, wangekitumia kuwashauri vyema viongozi ili kukijenga na kukiimarisha CCM.

Hata hivyo, sisi wengine ambao tunavitazama vyama vya siasa kama daraja na nyenzo ya kutusaidia kupata viongozi bora kwa ajili ya kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu, hatuoni muhari kusema kweli.

Hasa tunaoamini kwamba, bila CCM imara nchi yetu itayumba, tunashikwa na mzuka tukisikia ama kuona yuko

Rais Samia ni fursa, asitwezwe

Inatoka Uk. 16

kiongozi mahala kwa msembo wa Rais Samia ‘anapandisha mabega,’ kwakweli tunapata shida zaidi na kuamua kusema mtazamo wetu hadharani.

Hivi karibuni tumesikia kwamba kiongozi mmoja wa Uoja wa Wanawake wa CCM (UWT) ngazi ya mkoa ambaye ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, anatumia kugawa wanachama akidai hawakumuunga mkono kwenye uchaguzi mkuu wa chama uliopita?

Siyo picha nzuri kwa sababu CCM ni moja, na kiongozi yeyote wa jumuia za chama hicho tawala ana wajibu wa kuunganisha wanachama badala ya kuwabagua kimatabaka jambo ambalo linaweza kutweza heshima ya Mwenyekiti wa CCM Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amejipambanua kukijenga na kukiimarisha chama bila kumbagua yeyote.

Aidha, CCM kwa upande mwingine ndicho chama ambacho Watanzania wengi wamekiamini kukipa dhamana ya kuongoza nchi kwa kipindi cha miaka mitano kutoka 2020-2025, hivyo hatutarajii kwa vyovyote vile kiwe na viongozi wa jumuia wababaishaji na ‘wapandisha mabega’.

Inawezekana kabisa wakati wa mchujo wa kupata majina ya wagombea, vikao vilijiridhisha pasi na shaka ‘usafi’ wa mgombea wao na hivyo wakampitisha ili wajumbe halali wa mkutano mkuu wa uchaguzi wakafanye uamuzi.

Lakini, leo inapobainika kiongozi wa jumuia moja anamrubuni katibu wake wa mkoa kuchota fedha za jumuia bila utaratibu na anapoulizwa anajibu eti ni fedha zake alizozipata kwa njia zake na bado chama hakimuwajibishi, ni hatari kwa ustawi wa taasisi hiyo kubwa ya kisiasa.

Ikiwa taarifa zilizoenea ni za kweli, basi kwa maoni yangu ni fedheha kwa kiongozi wa jumuia yenye ‘Jeshi’ kubwa



Daniel Chongolo, Katibu Mkuu wa CCM

la wanawake, kumtupia maneno ya kumshushia hadhi katibu wake wa CCM ngazi ya mkoa mbele ya kikao chenye wajumbe wanaomheshimu, kwani kufanya hivyo ni sawa na kutweza heshima ya mwenyekiti wa chama hicho.

Ni aibu pia kushuhudia kiongozi mwenye kaliba hii kuzungumza maneno ya ovyo mbele ya kikao kilichohudhuriwa na viongozi wake wakiwemo kutoka ngazi za taifa.

Narudia tena, kama ni kweli, wanajumuia hiyo walio wengi kwenye mkoa huo uliopo Tanzania Buri wanamnung’unikia mwenyekiti wao UWT, kwanini CCM isiunde tume maalum ya kuchunguza ikapata majibu kuliko kuacha hali ya hewa ‘ikiendelea kuchafuka na kuwapa wapinzani agenda?’

Kabla sijaandika haya, nilifanya jitihada kumtafuta ‘Boss Lady’ huyo wa UWT mkoa na alinipa ushirikiano mzuri tu katika mazungumzo yetu ambapo licha ya kukanusha tuhuma hizo, lakini alikiri kuna tatizo mahala linalohitaji viongozi wa juu kuinglia kati.

Nimalizie kwa kusema kwamba, CCM wasipoziba ufa leo wajipange kesho kwenda kujenga ukuta.

Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa namba ya simu: 0784 43 85 46 au Email: mtagaluka@gmail.com.

Riwaya

Tetemeko la ndumba

Mtunzi: Innocent N. ZAGALLO

BINADAMU hawako sawa. Kila mmoja anapokuwa na umri mkunbwa huamua maisha yake yaweje. Pamoja na kuwa kila mmoja anapenda mafanikio, lakini hupitia njia tofauti kufikia “maisha bora.”

Wapo wanaotumia imani za dini, elimu, ujanja wa mjini, lakini wapo pia wanaotumia ndumba kufanikiwa.

Hadithi hii imebeba mengi juu ya matumizi ya “nguvu za giza” – yaani kuamini katika uchawi (ndumba) ili kufikia mafanikio. Wahusika wote na matukio ni ya kufikirika, hayana uhusiano na tukio wala mtu yeyote. Endelea...

MVUA ya rasharasha iliyoanza kunyesha tangu asubuhi mjini Kigoma, iliendelea hata usiku ulipotinga. Na hakukuwa na dalili ya kukatika au kupungua. Hilo halikuwa jambo la ajabu kwa kipindi hicho cha masika mvua kunyesha kwa zaidi ya saa 10. Lilikuwa ni jambo la kawaida.

Usiku huo, Mzee Songoro alikuwa nyumbani kwake, itongoji cha Mwanga, Mtaa wa Mabatini akisubiri mlo wa usiku uliokuwa ukiandaliwa na mkewe. Alikuwa ameketi sebuleni akitazama televisheni huku pia akisubiri taarifa ya habari.

Ilipotimu saa 2.00 kituo fulani cha televisheni kikaanza kutangaza taarifa ya habari, muhtasari ukiwa utangulizi wa habari yenyewe. Kwanza Mzee Songoro alishtuka, kisha akashangaa. Hakuyaamini masikio wala macho yake. Akatega masikio kwa makini na kukikodolea macho makali kioo cha televisheni.

Kisha habari kamili ikaanza;

Jambazi sugu aliyetuhumiwa kwa

makosa mbalimbali yakiwamo ya ubakaji, matumizi ya silaha na mauaji, Shaka Songoro, leo amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya mahakama kuridhika na maelezo ya upande wa mashtaka, ushahidi, hivyo kumtia hatiani...

Ilikuwa ni habari ndefu iliyoambatana na picha ya mtuhumiwa huyo. Na ikawa ni habari iliyomshtua na kumsononesha Mzee Songoro kwa kiasi kikubwa. Hakuendelea kuitazama televisheni hiyo wala kutega masikio kusikiliza habari nyingine.

Alinyanyuka na kuvuta hatua mbili akielekea jikoni, lakini mara akasita. Akarudi sofani na kujipweteka pwaa!

Akashusha pumzi ndefu. Kisha akaita kwa sauti kali: “Mama Shaka! Mama Shaka weee!”

Ilikuwa ni sauti iliyoyafikia masikio ya mkewe kwa usahihi, ikamshtua na kumshangaza. Akaacha kufanya alichokuwa akikifanya. Akaenda sebuleni huku akitweta.

“Vipi, baba Shaka?”

“Keti,” Mzee Songoro alimwamuru huku kakunja uso.

“Kuna nini baba Shaka, mbona unaniweka roho juu?” Mama Shaka alihoji huku akijipweteka sakafuni puu!

Mzee Songoro hakuwa na pupa ya kuzungumza. Alitulia na kushusha pumzi kwa nguvu. Kisha akaingiza mkono ndani ya mfuko wa koti lake jeusi na kutoa msokoto wa tumbaku.

Akauweka mezani na kuingiza tena mkono huo ndani ya mfuko wa suruali. Huko akatoa kibiriti. Akahema kwa nguvu na kumtupia jicho Mama Shaka. Akagundua kuwa amekumbwa na woga.

Itaendelea...

Kandanda

Ni wakati wa Stars Afcon



Na Nestory NESTORY

BAADA ya Timu ya Taifa ya Tanzania “Taifa Stars” kujihakikishia nafasi ya kushiriki michuano mikubwa ya soka Afrika (Afcon), furaha ya wapenzi wa kandanda imedhihiri.

Idadi kubwa ya wananchi wanaoendelea kusimulia mechi ya mwisho ya Taifa Stars dhidi ya Algeria kwa namna ilivyochezwa; wapo wanaosema timu ya Tanzania ilicheza chini ya kiwango na wengine wanadai ilicheza zaidi kujihami.

Wote wanaosema hayo huenda wako sahihi kwa mujibu wa uchambuzi wao, lakini kitu kikubwa zaidi ni kwamba Taifa Stars wamefuzu kuingia kwenye michuano ya Afcon.

Taifa Stars ikiwa chini ya Kocha Adel Amrouche sasa itashiriki Afcon 2023.

Furaha na faraja kwa Watanania imeonyeshwa hadi na Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye pamoja na kwuapongeza wachezaji wa Taifa Stars, benchi la ufundi na watu wengine

waliofanikisha maandalizi ya timu hiyo, pia alitoa Sh. milioni 500.

Kiasi hicho cha fedha kimetolewa ikiwa ni pongezi, lakini kikubwa zaidi ni kuwapa msukumo wa kujiandaa vyema kwa mashindano ya Afcon, ambayo siyo mepesi kwa kuwa yanakutanisha timu kubwa na zenye uzoefu wa michuano migumu ya kimataifa.

Kupenya kwa Stars hadi kutinga Afcon – baada ya kutoka sare (0-0) dhidi ya Algeria, kunaweka rekodi sawa kwamba hii ni mara ya tatu kwa timu hiyo kushiriki michuano hiyo.

Tanzania ambayo ilishiriki Afcon mwaka 1980 na 2019 imekamilisha michezo ya Kundi F ikiwa na pointi nane ikiwa inazidiwa na Algeria yenye pointi 16 ambayo nayo imefuzu.

Uganda iliyokuwa imekamia kupenya, imebaki na pointi 7, baada ya kuifunga Niger kwa mabao 2-0.

Michuano hiyo inayosubiriwa kwa hamu kubwa na wapenzi wa soka, inatarajiwa kufanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, 2024 nchini Ivory Coast.

PICHA YA PAMOJA...



Aliyekuwa Mbunge wa Mikumi na mwanamuziki mahiri, Joseph Haule, almaarufu kwa jina la “Profesa J,” juzi – Jumamosi, alikwenda kumsabahi Rais wa Nne wa Tanzania, Jakaya Kikwete nyumbani kwake Kawe, Dar es Salaam. (Picha na Ofisi ya Rais Mstaafu).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

